# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO NGOME

**(NGOME SACCOS LTD)**

**DSR 991**

# SERA YA MIKOPO

**TOLEO LA II: 2020**

# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO NGOME

**(NGOME SACCOS LTD)**

**DSR 991**

# SERA YA MIKOPO

**TOLEO LA II: 2020**

## YALIYOMO


**SEHEMU YA KWANZA** .......... 5
1.0 Historia ya Chama .......... 5
1.1Utangulizi .......... 5
1.2 Mgawanyo wa madaraka .......... 6
1.3 Madhumuni ya Sera ya Mikopo .......... 7
1.4 Walengwa wa sera hii .......... 8

**SEHEMU YA PILI** .......... 8
2.0 Aina za mikopo
2.1 Utoaji wa mikopo na taarifa ya kukataliwa kupewa mkopo .......... 8
2.2 Utoaji wa mikopo kwa wanachama .......... 8
2.3 Sifa za mwanachama anayestahili kupata mkopo .......... 9
2.4 Maombi ya mkopo .......... 11
2.5 Mrejesho wa sababu za kukataliwa kupewa mkopo .......... 11
2.6 Mkopo juu ya mkopo .......... 12

**SEHEMU YA TATU** .......... 13
Gharama za Mkopo .......... 13
3.1 Riba, Ada na Adhabu za mikopo .......... 13

**SEHEMU YA NNE .......... 14**
4.0 Kinga dhidi ya majanga ya mkopo .......... 14
4.1 Gharama za kinga ya majanga ya Mkopo .......... 14
4.2 Taratibu za kuhudumia mfuko wa bima .......... 14

**SEHEMU YA TANO** .......... 15
5.0 Muda wa ukomo wa marejesho ya mkopo .......... 15
5.1 Ukomo wa kurejesha mkopo .......... 15

**SEHEMU SITA** .......... 16
6. 0 Vyanzo vya kukopesha na Ukomo wa Ukopeshaji .......... 16

6.1 Vyanzo vya Fedha za kukopesha; ........ 16
6.2 Ukomo wa ukopeshaji kwa kila aina ya mkopo ........ 16

**SEHEMU YA SABA** ........ 17
7.0 Uidhinishwaji na Urejeshaji wa Mikopo ........ 17
7.1 Uidhinishaji wa maombi ya mikopo ........ 17
7.2 Viwango vya mikopo na uidhinishaji ........ 18
7.3 Uidhinishaji wa Bodi ya Chama ........ 19
7.4 Mikopo kwa viongozi ........ 19
7.5 Mikopo kwa watendaji wa chama ........ 19
7.6 Mikopo shirikishi (Loan Participation) ........ 20
7.7 Urejeshaji wa mikopo ........ 20
7.8 Marejesho ya mikopo ........ 20

**SEHEMU YA NANE** ........ 22
8.0 Ukokotoaji na uainishaji wa mikopo iliyocheleweshwa ........ 22
8.1 Taarifa za kuainisha mikopo iliyocheleweshwa ........ 22

**SEHEMU YA TISA** ........ 23
9.0 Usitishaji wa mapato tarajiwa na marekebisho ya mkopo ........ 23
9.1 Usitishwaji wa mapato tarajiwa kutoka mikopo cheleweshwa .. 23
9.2 Mapitio ya kufanya marekebisho ya mikopo ........ 23

**SEHEMU YA KUMI** ........ 24
10.0 Madeni, Matengo na Usimamishaji wa Mikopo kwa Muda ........ 24
10.1 Madeni Mabaya ........ 24
10.2 Matengo ya madeni mabaya ........ 24
10.3 Kusimamisha mikopo kwa muda ........ 25

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA** ........ 26
11.0 Ukusanyaji wa Madeni ........ 26
11.1 Mambo ya kuzingatia kabla ya kukusanya madeni ........ 26
11.2 Mkataba wa mkusanya madeni ........ 27

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI** .................................................. 28
12.0 Ufutaji wa Mikopo na Uuzaji wa Dhamana .............................. 28
12.1 Hatua za ufutaji wa mikopo .............................................. 28
12.2 Taratibu za chama kuuza dhamana za mwanachama ............ 29
13.0 HITIMISHO ................................................................................ 30

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 HISTORIA YA CHAMA

NGOME SACCOS LTD yenye nambari ya usajiri DSR 991 ilisajiliwa tarehe 30 April 2007, chini ya sheria ya Ushirika No. 20 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2004, kama inavyorejewa na sheria ya sasa ya Ushirika No. 6 ya mwaka 2013 na kanuni za Huduma ndogo za fedha za SACCOS za Mwaka 2019 . Wanachama wa Ngome SACCOS Ltd wanatokana na Fungamano la Pamoja, Maafisa ,Maaskari , Wastaafu pamoja na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wale waliohamia wizara nyingine wakiwa wanachama Hai wa Ngome SACCOS.

## 1.1 UTANGULIZI

Sera ya Utoaji, ukusanyaji na ufutaji wa mikopo ya NGOME SACCOS ni mwongozo uliowekwa na chama kwa ajili ya kusimamia namna ya utoaji wa mikopo ndani ya chama kwa Maafisa, Askari na Wastaafu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Watumishi wa Umma toka wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga taifa pamoja na watumishi wa umma waliohamia wizara nyingine wakiwa bado ni wanachama wa Ngome SACCOS kwa nia ya kupiga vita umasikini na kuboresha hali ya maisha yao, familia zao na jamii kwa ujumla. Taratibu hizi za mikopo zimetungwa kwa kuzingatia misingi ya kanuni za utendaji bora wa chama na lazima zifuatwe na zitumike katika shughuli zote za utoaji mikopo kwa wanachama.

Sera hii itazingatia matakwa ya Sheria ya Huduma ndogo za fedha Na.10 ya mwaka 2018 na Kanuni za Huduma ndogo za fedha za mwaka 2019. Sera hii imejumuisha Maeneo yote muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika usimamizi wa mikopo ikiwa ni pamoja na utoaji wa mikopo, Ukusanyaji wa Mikopo, Ufutaji wa Mikopo, Dhamana za mkopo, taratibu za kuuza dhamana, bima ya mikopo, kama zinavyoelekezwa katika Kanuni ya 28-43 ya Kanuni za SACCOS za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.

Sera hii imejumuisha Sehemu kumi na mbili. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili ni utoaji wa mikopo na taarifa ya kukataliwa kupewa mkopo, sehemu ya tatu ni gharama za mkopo, sehemu ya nne ni bima ya mkopo, sehemu ya tano ni muda kikomo wa marejesho ya mkopo, sehemu ya sita ni vyanzo vya kukopesha na ukomo wa ukopeshaji, sehemu ya saba ni uidhinishaji wa maombi ya mkopo na urejeshaji wa mkopo, sehemu ya nane ni ukokotoaji na uainishaji wa mikopo iliyocheleweshwa, sehemu ya tisa usitishaji wa mapato tarajiwa wa marekebisho ya mkopo, sehemu ya kumi ni madeni, matengo na usimamishaji wa mikopo kwa muda, sehemu ya kumi na moja ni ukusanyaji wa madeni, sehemu ya kumi na mbili ni ufutaji wa mkopo na uuzaji wa dhamana.

Sera hii imeandaliwa kwa kuzingatia sharti Na.64 la masharti ya chama, pamoja na mambo mengine sera itapitiwa mara kwa mara ili kuona kama kunahitajio la kufanya maboresho na bodi itakuwa na jukumu la kuwasilisha maoni na mapendekezo watakayoona yanafaa kwa lengo kuridhiwa na mkutano mkuu kabla ya kufanya maboresho.

## 1.2 Mgawanyo wa madaraka

a. **<u>Bodi ya Chama</u>**

Ndiye msimamizi mkuu wa Mikopo. Itapata taarifa za mikopo mara kwa mara kadri itakavyohitaji kutoka kwa Kamati ya Mikopo.

b. **<u>Kamati ya Mikopo</u>**

(i) Itakuwa na dhamana ya kutoa/kuidhinisha/kusimamia mikopo kwa kuzingatia Sera na Kanuni za utoaji mikopo.
(ii) Kamati itapata mapendekezo/maoni/ushauri juu ya mikopo toka kwa Meneja Mikopo.
(iii) Itawajibika kwa Bodi ya Chama.
(iv) Kamati inaweza kukasimu baadhi ya madaraka yake kwa Meneja mkuu au Meneja Mikopo baada ya kupata kibali cha bodi kwa mfano kupitisha/kuidhinisha mikopo ya dharura.

c. **<u>Idara ya mikopo</u>**

**Meneja Mikopo**

Ndiye mtendaji mkuu wa shughuli za kila siku za mikopo Chamani. Atawajibika kwa Kamati ya Mikopo na anaweza kukasimu baadhi ya madaraka yake kwa wasaidizi wake mfano; Afisa Mikopo, Data entry, Credit Quality Control baada ya kupata kibali kutoka Kamati ya Mikopo.

d. **Majukumu ya Meneja Mikopo**

i) Kufanya utafiti ili kujua mahitaji halisi ya mikopo kwa wanachama wa NGOME SACCOS LTD.

ii) Kuchukua hatua za kupata mawasiliano ya wanachama wote wanaotarajia kukopa na wakopaji wote.

iii) Kukutana na kutoa ushauri kwa wanachama wanaohitaji kukopa ili kujua mahitaji yao halisi ya mikopo na uhai wa kiuchumi wa miradi yao.

iv) Kutembelea maeneo wanayofanyia kazi na kukusanya taarifa za mwanzo kuhusu ustawi wa miradi na dhamana za mikopo ya wakopaji.

v) Kuchambua fomu za mikopo na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Mikopo kuhusu uwezo wa mkopaji kurejesha mkopo na namna atakavyorejesha.

vi) Kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Mikopo/Meneja Mkuu juu ya maendeleo ya miradi ya wakopaji.

vii) Kufuatilia marejesho ya mikopo na kuhakikisha kwamba mikopo yote inalipwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

viii) Kupitia taarifa za marejesho ya mikopo kila mwezi ili kugundua mikopo iliyocheleweshwa au iliyosimama na kuchukua hatua zinazostahili kwa wahusika.

## 1.3 Madhumuni ya Sera ya Mikopo

(a) Kuweka misingi na kanuni bora za utoaji mikopo.

(b) Kuepusha migongano isiyo ya lazima katika kutoa mikopo.

(c) Kupunguza hatari ya mikopo mibaya.

(d) Kujenga imani kwa taasisi za ndani na nje ya chama, wanachama na wasio wanachama kwa ujumla.

(e) Kuiwezesha Bodi katika usimamizi wa mikopo.

(f) Kutekeleza kwa vitendo sheria ya Ushirika namba 6 ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2014 na 2015, Sheria ya Huduma ndogo za fedha Na.10 ya mwaka 2018 na Kanuni zake za Huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.

## 1.4 Walengwa wa sera hii

### 1.4.1 Wadau wa ndani

(i) Wanachama ndio walengwa wakuu wa Sera hii kwa kuwa ndio wakopaji

(ii) Watendaji – Hawa ni wataalamu wa kuchanganua na kutathmini mikopo inayoombwa na inayotolewa.

(iii) Wajumbe wa bodi, Kamati ya usimamizi – watahusika katika kusimamia na kuhakikisha kuwa taratibu zote za Sera zinafuatwa.

### 1.4.2 Wadau wa nje

i) Wakaguzi wa nje – Watatumia Sera hii wakati wa ukaguzi.

ii) Maafisa ushirika – Ni washauri katika utekelezaji wa sera hii kama wawakilishi wa Serikali.

iii) Taasisi za Kifedha na wakopeshaji wengine – Watatumia sera hii wakati wa kutoa huduma ya mikopo chamani.

iv) Mrajis wa Vyama vya Ushirika – anahusika na kuidhinisha sera hii na kusimamia utekelezaji wake.

v) Makampuni ya kuchakata taarifa za wakopaji

vi) Waajiri

vii) Benki kuu ya Tanzania

viii) Tume ya Ushirika

ix) Wadau wengine

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UTOAJI WA MIKOPO NA TAARIFA YA KUKATALIWA KUPEWA MKOPO

### 2.1 Aina za Mikopo.

NGOME SACCOS itatoa mikopo ya aina mbali mbali kama ilivyoainishwa katika jedwali Na 1 hapo chini.

| Aina ya Mkopo | Riba | Njia ya ukokotozi | Muda wa marejesho |
|---|---|---|---|
| Maendeleo | 10 | "Reducing Balance Method" | Mwaka 1 hadi miaka 5 |
| Dharura | 20 | "Reducing Balance Method" | Mwezi 1-12 |
| Sikukuu | 10 | "Straight line method" | Miezi 3 |

### 2.2 Utoaji wa mikopo kwa wanachama

NGOME SACCOS itatoa mikopo kwa wanachama wote wenye sifa ya kupata mikopo kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukopesha na kwa kuzingatia sera ya mikopo ya chama bila kuathiri sheria ya Huduma ndogo za fedha na Kanuni za huduma ndogo za fedha zinazosimamia SACCOS za mwaka 2019.

### 2.3 Sifa za mwanachama anayestahili kupata mkopo

Ili kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha mikopo inatolewa baadhi ya mambo yafuatayo yatazingatiwa kabla mwanachama hajapatiwa mkopo ambapo mwanachama ni lazima awe na sifa zifuatazo;

(a) Awe mwanachama hai wa NGOME SACCOS anayechangia Akiba yake mara kwa mara kama inavyoelekezwa na sera ya akiba ya Chama, Mwenye Hisa zisizopungua kumi(10) zenye thamani ya Tshs 100,000 kama inavyoelekezwa na sera ya uhamasishaji uwekaji akiba amana na hisa.

(b) Awe ametimiza miezi mitatu chamani tangu kujiunga kabla ya kuomba huduma ya mkopo chamani.
(c) Asiwe na mkopo alioshindwa kulipa wakati wa kuomba mkopo mwingine.
(d) Asiwe na mkopo alioshindwa kulipa kutoka taasisi nyingine.
(e) Awe na historia nzuri chamani katika urejeshaji wa mikopo yake
(f) Awe mshiriki mzuri kwenye shughuli za chama
(g) Awe na mradi unaotengeneza faida.
(h) Awe na dhamana toshelevu. Awe na mdhamini au wadhamini ikiwa akiba zake, hisa za hiyari na amana hazijitoshelezi kudhamini mkopo anaoomba.

**Pamoja na sifa zilizoainishwa katika sehemu hii pia mambo yafuatayo yatazingatiwa kama sifa ya mwanachama kuweza kupatiwa mkopo.**

### 2.3.1Akiba,Hisa na Amana

Akiba, Hisa na Amana za mwanachama zilizowekwa chamani zitazingatiwa na kuwa kigezo muhimu cha kutoa mkopo kwa mwanachama na ikiwa mwanachama hajatimiza sharti la kuwa na hisa na kuweka akiba kama taratibu zinavyoelekeza katika sera ya uhamasishaji wa uwekaji akiba na hisa anaweza kukosa sifa ya kupata mkopo.

### 2.3.2Tabia (character)

Tabia ya mkopaji itatathiminiwa kikamilifu kulingana na kumbukumbu zake za ukopaji na urejeshaji wa mikopo yake. Wanachama, Kamati ya Usimamizi, Kamati ya mikopo au kiongozi yeyote wa chama anayeweza kuwa sehemu ya kujua tabia ya mkopaji na anaweza kutoa maoni juu ya mkopaji husika.

Dhamana kubwa iliyopita kiwango cha mkopo haitakuwa kigezo cha kumpa mkopo mwanachama aliye na tabia au historia mbaya katika ukopaji na urejeshaji wa mikopo.

Wakopaji wapya watatathiminiwa kwa kuzingatia uwezo wao wa kufanya marejesho na kuchambua mikopo yao kupitia taasisi za uchakataji wa taarifa za wakopaji (Credit reference bureau).

### 2.3.3hali (condition)

Hali ya utoaji wa mkopo kwa mwanachama itazingatia mambo ya nje yanayoathiri mkopo wa mwombaji ikiwa ni pamoja na

i. Hali ya uchumi wa nchi
ii. Thamani ya pesa
iii. Sheria za nchi
iv. Hali ya soko la biashara inayoombewa mkopo
v. Hali ya soko la kazi/ajira
vi. Na mambo mengine yanayoathiri hali ya urejeshaji mkopo.

### 2.3.4 Uwezo wa mtiririko wa kifedha

Uwezo wa kurejesha mkopo ndio kitu cha kwanza na cha msingi cha kuangalia katika kutathimini uwezo wa mwanachama kurejesha mkopo anaoomba kwa kutegemea shughuli za kiuchumi

### 2.3.5Dhamana ya mkopo (collateral)

Dhamana itakayowekwa/zitakazowekwa na mwanachama wakati wa kuomba mkopo zitatakiwa kuwa na thamani zaidi ya kiwango cha mkopo utakaoombwa. Aidha, tathmini halisi ya thamani ya dhamana itakayowekwa na wanachama itatakiwa kutathminiwa vizuri kabla ya kuwekwa kwenye dhamana ya mkopo. *(Mthaminishaji anayetambuliwa na serikali).*

## 2.4 Maombi ya Mkopo

Mwanachama kabla ya kupatiwa mkopo atapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

(a) Atachukua fomu chamani/mwakilishi ataijaza na kuirudisha chamani.

(b) Mwanachama atalipia gharama za fomu ya maombi ya mkopo kiasi cha shilingi 1,000 wakati wa kuchukua fomu au atakatwa kupitia katika mkopo alioomba.

(c) Mwanachama ataomba kiasi cha Mkopo kulingana na hitaji lake.

(d) Mwanachama atalazimika kuambatisha hati ya mshahara (payslip original), barua ya maombi ya mkopo,nakala ya kitambulisho cha kazi na picha 2 katika fomu ya mkopo.

(e) Ikiwa mwanachama atakopa kupitia dhamana zake toshelevu ataambatanisha nyaraka za dhamana hiyo.

(f) Atakuwa tayari kutoa ridhaa kwa chama kutoa taarifa zake za mikopo kwa mamlaka za uchakataji wa taarifa za wakopaji nchini pasipo hata kutaarifiwa.

## 2.5 Mrejesho wa sababu za kukataliwa kupewa mkopo

Kwa kuzingatia kanuni ya 32 ya Kanuni za huduma ndogo za fedha zinazosimamia SACCOS ya 2019, kamati ya mikopo itapaswa kumtaarifu mwanachama kwa maandishi ikiwa itaona mwanachama husika hajakidhi vigezo vya kupata mkopo ndani ya siku saba baada ya kufanya maamuzi ya kukataliwa mkopo huo.

## 2.6. Mkopo juu ya mkopo( top up loan)

Chama hakitokopesha top up loan isipokuwa pale tu kitakapoona ni muhimu kufanya hivyo kwa manufaa na ustawi wa chama, endapo kitaamua kutoa top up basi ni kwa mkopo wa maendeleo uliobakiza miaka miwili kuisha kwa mkopo wa muda wa miaka mitano(5) na mwaka mmoja kwa mkopo wa miaka mitatu(3).

## SEHEMU YA TATU

## GHARAMA ZA MKOPO

### 3.1 Riba, Ada na Adhabu za mikopo

Kiwango cha riba, ada, adhabu na gharama nyingine za mikopo vitapendekezwa na Bodi ya Chama na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa wanachama. Aidha, kiwango cha riba kitawekwa baada ya kufanyika uchambuzi maalum utakaonyesha kiwango cha riba kilichowekwa kitanufaisha wanachama na kuweza kumudu gharama za uendeshaji wa shughuli za chama na mahitaji mengine ya chama kwa kuzingatia ulazima uliopo.

viwango vya riba, ada, adhabu na gharama nyingine vitafanyiwa marejeo ya mara kwa mara ili kuona kama vinaendana na wakati na vinaweza kubadilishwa baada ya kuridhiwa na mkutano mkuu na kuidhinishwa na Mrajis.

Mikopo yote italipiwa riba kwa kila mwezi kama inavyofafanuliwa kwenye Sera hii kwa kuzingatia jedwali Na.2

**Jedwali Na.2 Viwango vya Ada, Riba na Adhabu**

| Aina ya Mkopo | Bima ya mkopo | Ada ya Mkopo | Riba (%) | Adhabu (%) x Rejesho lilocheleweshwa |
|---|---|---|---|---|
| Maendeleo | **1%** | **1%** | **10** | **Nil** |
| Sikukuu | **0** | **1%** | **10** | **Nil** |
| Dharura | **0** | **1%** | **20** | **Nil** |

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 KINGA DHIDI YA MAJANGA YA MKOPO

### 4.1 Gharama za kinga ya majanga ya Mkopo

NGOME SACCOS itatoza kiasi cha 1% katika kila mkopo unaochukuliwa isipokuwa mkopo wa dharura na kiasi hicho kitahifadhiwa katika akaunti maalum kwa lengo la kulinda mikopo ambayo haitarejeshwa kutokana na sababu zifuatazo;

a. Ikiwa mwanachama amefariki akiwa hajamaliza mkopo na chama kimethibitisha kifo chake.

b. Ikiwa mwanachama amepata ulemavu wa kudumu na imepelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kumwingizia kipato na hatimaye kushindwa kulipia mikopo anayodaiwa

c. Ikiwa mwanachama amerukwa na akili na hawezi kutoa ushirikiano katika kufanya marejesho kwa mujibu wa mkataba wake na daktari wa serikali amethibitisha juu ya ugonjwa wa akili wa mwanachama husika.

### 4.2 Taratibu za kuhudumia mfuko wa bima

a. Fedha za mfuko wa bima ya mkopo zitawasilishwa benki katika akaunti maalum mara baada ya mwanchama kupatiwa mkopo

b. Fedha za mfuko zitatumika kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuzingatia mahitaji yatayojitokeza.

c. Ikiwa mfuko haujaimarika vya kutosha kuweza kumudu mahitaji yanayojitokeza kiasi kinachodaiwa kinaweza kusubiri mfuko uimarike ndipo kilipwe

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MUDA WA UKOMO WA MAREJESHO YA MKOPO

### 5.1 Ukomo wa kurejesha mkopo

Mwanachama atarejesha mkopo wake kwa utaratibu aliopangiwa na kwa namna yeyote ile muda wa juu wa kurejesha mkopo hautazidi miaka mitano.

**Jedwali Na. 3 Aina ya mikopo na muda wa marejesho**

| Aina ya Mkopo | Muda wa marejesho |
|---|---|
| Maendeleo | Mwaka 1 hadi miaka 5 |
| Dharura | Mwezi 1-12 |
| Sikukuu | Miezi 3 |

## SEHEMU YA SITA

## 6. 0 VYANZO VYA UKOPESHAJI NA UKOMO WA MIKOPO

### 6.1 Fedha za kutoa mikopo chamani zinaweza kutoka katika maeneo yafuatayo;

a. Hisa za hiari za wanachama
b. Akiba za wanachama
c. Malimbikizo ya faida
d. Mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha na zisizo za kifedha.
e. Misaada kutoka kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi.(kwa kuzingatia masharti)

### 6.2 Ukomo wa ukopeshaji kwa kila aina ya mkopo

Kiwango cha juu katika kila mkopo bila kuathiri matakwa ya kanuni ya 33(1) ya Kanuni za huduma ndogo za fedha itakuwa kama ifuatavyo.

a. Maendeleo - milioni sabini(mil 70)
b. Dharula- milioni mbili( mil 2)
c. Mikopo ya sikukuu- milioni moja(mil 1)

## SEHEMU YA SABA

# 7.0 UIDHINISHWAJI NA UREJESHAJI WA MIKOPO

## 7.1 Uidhinishaji wa maombi ya mikopo

a. SACCOS haitatoa mkopo bila idhini ya kamati ya mikopo
b. Kamati ya mikopo haitaidhinisha mkopo kama mkopo haijadhaminiwa kikamilifu.
c. Kamati ya mkopo itaridhia ombi la mkopaji kupewa mkopo baada ya kujiridhisha na uwezo wa mwanachama kufanya marejesho
d. Kamati ya mikopo ina haki ya kukataa/kukubali au kurudisha ombi la mkopo kwa mwanachama ikiwa mwanachama atakuwa hakutimiza vigezo vya kupewa mkopo kama ilivyoelekezwa katika sehemu ya 2.1 ya sera hii.
e. Ikiwa ombi la mkopo halijakubaliwa, SACCOS itamfahamisha mwanachama sababu za kukatatiliwa kwa ombi lake ndani ya kipindi cha siku saba tangu fomu kupokelewa.
f. Fedha za mikopo zitatolewa kutegemeana na hali ya ukwasi chamani lakini kwa namna yeyote ile mikopo midogo itapewa kipaumbele na ikiwa hali ya ukwasi wa chama iko chini.
g. Kamati ya mikopo haitaidhinisha kiwango cha mikopo kinachozidi shilingi milioni Thelathini( mil 30)
h. Kamati ya kitaalamu haitaidhinisha kiasi cha mikopo kinachozidi shilling milioni mbili(mil 2)
i. Kiasi cha mkopo kinachozidi shilingi milioni thelathini (milioni 30) kitaamuliwa na bodi ya chama.
j. Meneja wa chama au Meneja Mikopo anaweza kukasimiwa kuidhinisha mikopo yote ya dharura kwa wanachama wenye sifa za kukopa mara baada ya afisa mikopo kujiridhisha uwezo wa mkopaji katika kurejesha mkopo husika wa dharura.
k. Kamati ya mikopo/kamati ya kitaalam itatumia kumbukumbu zifuatazo ili kufikia uamuzi wake;

i) Mali anazotumia mwanachama kudhamini mkopo
ii) Daftari linaloonyesha orodha ya wanachama
iii) Uzoefu katika shughuli anayoombea mkopo
iv) Aina ya mradi unaoombewa mkopo
v) Mahali mradi ulipo
vi) Pamoja na vigezo vingine vitakavyowekwa na chama.
vii) Kanuni ya 30 ya huduma ndogo za fedha za mwaka 2019

l. Kila mwanachama hatakopeshwa zaidi ya mikopo miwili ya maendeleo na ana haki ya kupewa mkopo wa dharula kama ikibidi. Aidha hatakopeshwa mkopo wa pili hadi awe amerejesha mkopo wa awali kwa muda usiopungua miezi sita(6).

NB; Masharti tajwa hayamzuii mwanachama kukopa mikopo(product) ya mahitaji maalum. Mfano mkopo wa sikukuu, kama hali ya fedha ya chama inaruhusu.

## 7.2 Viwango vya mikopo na uidhinishaji

### 7.2.1 Uidhinishaji wa kamati ya mikopo

Uidhinishaji wa mikopo utakua chini ya kamati ya mikopo au kamati ya kitaalam na itaidhinisha mkopo usiozidi kiasi cha shilingi milioni thelathini (mil. 30).

### 7.2.2 Uidhinishaji wa Meneja Mkuu

Meneja Mkuu wa NGOME SACCOS anaweza kukasimiwa kuidhinisha mikopo ya dharura baada ya Afisa mikopo kujiridhisha kama mkopaji anaweza kufanya marejesho kwa mkopo huo, mikopo mingine itafuata taratibu zilizoainishwa katika sera hii.

### 7.2.3 Uidhinishaji wa Bodi ya Chama

Bodi itakuwa na jukumu la kuidhinisha mikopo yote inayozidi kiasi cha shilingi milioni thelathini(mil.30) ambayo kamati ya mikopo, kamati ya

kitalaam na menejimenti hawawezi kuidhinisha kama ilivyoelekezwa katika sera hii.

### 7.3 Mikopo kwa viongozi

a. SACCOS haitatoa mkopo kwa mjumbe wa bodi au mjumbe wa kamati yeyote kabla ya kupata idhini kutoka kwa wajumbe wa bodi.
b. Mjumbe wa bodi au wa kamati hatoruhusiwa kuwa miongoni wa wajumbe wa kikao wakati wa kupitisha mkopo wake.

### 7.4 Mikopo kwa Wastaafu

a. SACCOS itatoa mikopo kwa wastaafu kama wanachama wengine.
b. Wastaafu watafanya marejesho yao kupitia, pensheni zao, standing order, kulipa fedha taslimu katika akaunti ya chama au kwa kuweka dhamana ya mali isiyohamishika.

### 7.5 Mikopo shirikishi (Loan Participation)

a. NGOME SACCOS kwa kuzingatia Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha, inaweza kukopa kutoka SACCOS nyingine au kukopesha SACCOS kwa lengo la kuongeza ukwasi katika chama.
b. NGOME SACCOS itafuata taratibu zote za ukopaji na ukopeshaji kama zilivyoainishwa katika kanuni za Huduma Ndogo za fedha za mwaka 2019 na mikopo inayoombwa na chama kingine itafanyiwa tathmini na kamati ya mikopo na kupelekwa kwenye bodi ya chama kwa ajili ya kufanya maamuzi ya mwisho.
c. Iwapo Bodi itaidhinisha mkopo shirikishi, taratibu zote zinazopaswa kuzingatiwa na mkopaji na mkopeshaji zitazingatiwa kwa kuhakikisha panakuwepo na Mkataba wa

mkopo husika. aidha kiwango cha riba kwa SACCOS shirikishi kitakuwa cha makubaliano kutegemeana na soko la fedha.

**N.B,**

**Kwa namna yeyote ile SACCOS haitatoa mkopo kwa upendeleo, kwa viwango tofauti vya riba tofauti na vile anavyotozwa mwanachama mwingine.**

## 7.6 Urejeshaji wa mikopo

a. Mwanachama atafanya marejesho ya mkopo pamoja na riba kwa kupitia akaunti ya chama na kama kutakuwa na mazingira ya kukosekana kwa huduma ya benki katika eneo husika mwanachama anaweza kuwasilisha fedha taslimu ofisini muda wa kazi.

b. Mwanachama anaweza kulipa mkopo wake kabla ya muda wa mwisho kufika katika muda wa kazi bila kulipishwa adhabu

c. Ikiwa mwanachama atalipa kiasi cha mkopo wake au kulipa mkopo wote kwa mkupuo hatapaswa kulipa riba ya muda ambao hakukaa na mkopo kama inavyoelekezwa na kanuni ya 37(2) ya kanuni za SACCOS za mwaka 2019.

## 7.7 Marejesho ya mikopo

a. Kila mwanachama ana wajibu wa kuhakikisha anafanya marejesho yake kwa mikopo aliyochukua chamani.

b. Kamati ya Mikopo/Meneja Mkuu atahusika mara kwa mara kutengeneza taarifa ya hali halisi ya mikopo ya wanachama kila mwezi ili kutoa hali halisi ya mikopo inayohitaji kufuatiliwa kwa karibu zaidi.

c. Taarifa zitaonyesha hali halisi ya maendeleo ya mikopo na zitawasilishwa mbele ya Bodi kila baada ya robo mwaka na kuwekwa kwenye mbao za matangazo na sehemu ambazo wanachama wanapatikana.

d. Wadhamini wa mkopo watatakiwa kuhakikisha mkopaji anarejesha marejesho yake kwa mujibu wa jedwali la marejesho yake.

## SEHEMU YA NANE

## 8.0 UKOKOTOAJI NA UAINISHAJI WA MIKOPO ILIYOCHELEWESHWA CHAMANI.

Chama kitaandaa taarifa za ukokotoaji wa mikopo iliyocheleweshwa kwa kuanzia tarehe ya mwisho ambayo rejesho la mkopo husika lilifanyika mpaka pale malipo yote yatakapokuwa yamekamilika. Mikopo iliyocheleweshwa itakokotolewa kila mwezi na kutolewa taarifa siku ya mwisho wa mwezi ambapo mikopo hiyo itaainishishwa katika makundi yafuatayo:-

**Jedwali Na.4 Makundi na Hali ya Ucheleweshaji.**

| Na. | Makundi ya Uchelewaji | Hali ya Uchelewaji |
|---|---|---|
| 1. | Mikopo iliyopo kwenye angalizo | Siku 31-90 |
| 2. | Mikopo iliyo chini ya Kiwango | Siku 91-180 |
| 3. | Mikopo yenye mashaka | Siku 181-365 |
| 4. | Mikopo mibaya/Hasara | Zaidi ya siku 365 |

### 8.1 Taarifa muhimu zinazopaswa kuainishwa kwa mikopo iliyocheleweshwa

Taarifa ya ucheleweshwaji wa mikopo itajumuisha mambo yafuatayo;

a. Jina la mwanachama, anuani na mawasiliano yake binafsi
b. Tarehe mkopo ulipotolewa
c. Mkopo halisi uliotolewa na bakaa la deni linalodaiwa ambalo halijarejeshwa chamani
d. Majina ya wadhamini na dhamana ya mkopo iliyowekwa.

## SEHEMU YA TISA

### 9.0 USITISHAJI WA MAPATO TARAJIWA NA MAREKEBISHO YA MKOPO

### 9.1 Kusitisha mapato tarajiwa kutokana na mikopo iliyocheleweshwa

Chama kitasitisha riba zote tarajiwa ambazo zitakuwa zimekadiriwa kupatikana kwenye mwaka husika kutokana na mikopo iliyocheleweshwa iwapo mkopo uliotolewa hautalipwa kwa siku tisini. Aidha, chama kitaondoa mapato tarajiwa yanayotokana na mikopo kutoka katika akaunti ya mapato tarajiwa.

### 9.2 Mapitio ya kufanya marekebisho ya mikopo

NGOME SACCOS haitafanya marekebisho ya mkopo zaidi ya mara moja kwa wanachama wake watakaopewa mikopo na kushindwa kurejesha kwa wakati.

a. Mkopo wowote ambao umefanyiwa marekebisho au mabadiliko katika masharti yake ya awali, hautapaswa kuainishwa kama "upo katika daraja zuri" isipokuwa marejesho ya mkopo huo yamefanyika kikamilifu angalau mara nne mfululizo tangu mkopo ulipofanyiwa marekebisho.

b. iwapo mkopo utafanyiwa marejesho kikamilifu mara nne mfululizo, mkopo huo utaainishwa kama mkopo usiocheleweshwa.

c. NGOME SACCOS itatoa taarifa ya mikopo yote iliyofanyiwa marekebisho kama taarifa inayojitegemea katika mizania ya hesabu ya chama.

## SEHEMU YA KUMI

## 10.0 MADENI, MATENGO NA USIMAMISHAJI WA MIKOPO KWA MUDA

### 10. 1 Madeni Mabaya

a. Madeni mabaya ni yale yatakayokuwa yameshindwa kurejeshwa katika kipindi kinachozidi siku 30 kama ilivyofafanuliwa katika kanuni ya 40 (1)(2) ya kanuni za huduma ndogo za fedha (SACCOS) za mwaka 2019

b. Madeni mabaya yatafutwa katika mahesabu ya chama yatakapokuwa yamefikia zaidi ya miezi kumi na mbili (12) kwa kuzingatia Kanuni ya 43 ya kanuni za SACCOS za mwaka 2019.

c. Chama kitaendelea kufuatilia madeni hayo na yakilipwa yataingizwa kama mapato mengineyo kwa kuzingatia taratibu za kihasibu.

### 10.2 Matengo ya madeni mabaya

Chama kitafanya matengo ya mikopo mibaya kwa kuzingatia kanuni Na. 40(3) ya kanuni za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.
NGOME SACCOS itatenga kiasi toshelevu cha fedha kutoka katika faida yake ya mwaka kwa ajili ya kufidia mikopo mibaya iliyocheleweshwa na wanachama kwa kuzingatia kanuni Na. 40(3) ya kanuni za huduma ndogo za Fedha (SACCOS) za mwaka 2019
ili kufidia kiasi cha mikopo hiyo mibaya kama inavyoainishwa katika jedwali Na.2

**Jedwali Na.5 Matengo ya Mikopo Mibaya.**

| Na. | Makundi ya Uchelewaji | Hali ya Uchelewaji | Kiasi cha matengo(% ya bakaa kwa mkopo uliochelewa) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mikopo iliyopo kwenye angalizo | Siku 31-90 | 10% |
| 2. | Mikopo iliyo chini ya Kiwango | Siku 91-180 | 30% |
| 3. | Mikopo yenye mashaka | Siku 181-365 | 50% |
| 4. | Mikopo mibaya/Hasara | Zaidi ya siku 365 | 100% |

**Kiasi cha tengo litakalotengwa kwa ajili ya kufidia mikopo mibaya iliyocheleweshwa kitawekwa kwenye akaunti maalum ya mikopo mibaya.**

## 10.3 Kusimamisha mikopo kwa muda

a. Chama kinaweza kusimamisha utoaji wa mikopo kulingana na mwenendo wa ulipaji wa mikopo hiyo.

b. Ikiwa Mikopo mingi ambayo ipo mikononi mwa wanachama na haijakusanywa na hivyo kuhatarisha hali ya ukwasi katika chama "liquidity crisis".

c. Endapo Mrajis wa Vyama vya Ushirika atafanya ukaguzi na kubaini na kujiridhisha kuwa hali halisi ya kifedha ni mbaya.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

## 11. 0 UKUSANYAJI WA MADENI

Mikopo yote itakayotolewa na chama kwa wanachama wake itapaswa kulipwa chamani kwa utaratibu uliopangwa na ikiwa utataratibu uliowekwa hautafuatwa na wakopaji chama kitakuwa na jukumu la kufuatilia na kuhakikisha madeni yote yanakusanywa.

### 11.1 Mambo ya kuzingatia kabla ya kuanza ukusanyaji wa madeni

Chama kitaendelea kuhakikisha madeni yote yanakusanywa kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kati ya mkopaji na mkopeshaji na mambo yafuatao yakibainika ufuatiliaji wa karibu utahitajika, aidha miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na;

a. Malipo ya marejesho ya mwanachama yatakuwa pungufu ya malipo yaliyotakiwa kulipwa kwa mujibu wa masharti ya mkataba uliosainiwa na mwanachama kipindi anachukua mkopo.
b. Endapo malipo ya marejesho ya mwanachama hayatafanyika ndani ya kipindi cha siku thelathini (30) tangu marejesho hayo kutakiwa kufanyika bila kujali kuwa mkopo uliocheleweshwa ni riba au riba na mkopo msingi.
c. Iwapo Jedwali la marejesho ya Mkopo lililopo kwenye fomu ya mikopo halitazingatiwa katika marejesho ya mkopo ya mwanachama.

## 11.2 Mkataba wa mkusanya madeni

Chama kinaweza kuingia mkataba na mkusanya madeni endapo itaonekana mkopaji amecheleweshа marejesho na jitihada za chama kufanya ufatiliaji zimeshindwa kuzaa matunda na hatimae kuona umuhimu wa kuweka mkusanya madeni.

Aidha chama kinapaswa kuzingatia mambo yafuatayo kabla ya kuingia mkataba na mkusanya madeni;

a. Kuhakikisha mkusanya madeni ana kibali maalum cha kufanya kazi hiyo kutoka mamlaka halali za serikali (TCDC)
b. Kujiridhisha mahali na sehemu mtoa huduma anafanyia kazi zake
c. Kuangalia historia ya mtoa huduma
d. Kuhakikisha mtoa huduma analinda haki za mwanachama wakati wa kukusanya madeni
e. Kuhakikisha mkusanya madeni anakusanya deni kwa kuzingatia mkataba na makubaliano yaliyopo kwenye fomu ya mkopo na mkataba wa mkopo
f. Kuhakikisha mkusanya madeni anatambua vema mali za mkopaji zilizotumika kudhamini mkopo
g. Kufanya tathmini na kujirdhisha kama Kuhakikisha mkusanya madeni ana uwezo na vifaa vitakavyomsaidia kufanya kazi hiyo pasipo kuingiza chama gharama
h. Mkataba uainishe haki na wajibu wa pande zote na upite kwa mwanasheria kwa ajili ya kulinda haki za pande zote
i. Mkataba wa mkusanya madeni na chama unapitishwa kwa Mrajis ili aone kama mkataba husika haujaegemea upande mmoja
j. Kuhakikisha taratibu zote zitakazochukuliwa na Mkusanya madeni, zinalinda haki ya mwanachama na chama kwa ujumla

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

## 12.0 UFUTAJI WA MIKOPO NA UUZAJI WA DHAMANA

### 12.1 Hatua za ufutaji wa Mikopo

NGOME SACCOS itafuta mikopo yake kutoka katika mizania yake endapo:

a. Mkopo utacheleshwa kurejeshwa kwa zaidi ya siku 365;
b. Chama kitapoteza haki zake za kimkataba zinazohusiana na mkopo husika;
c. Chama kimekosa haki kisheria katika dai la mkopo husika
d. Mkopo utakapoonekana hauwezi kukusanywa;
e. Hakuna uwezekano wa chama kukusanya mkopo kutokana na hukumu ya mahakama.
f. Dhamana zote zilizodhamini mkopo, zimetathiminiwa na kuuzwa, na mapato yanayotokana na mauzo yameshindwa kufuta mkopo unaodaiwa
g. Chama hakina uwezo wa kukusanya mkopo au hakuna dhamana au jitihada za kukusanya deni zimeshindikana.
h. Ikiwa chama kina tengo la mikopo mibaya linalotosha kufuta mkopo

**N.B**

**Iwapo mkopo wa mwanachama utafutwa kwenye vitabu vya chama na kama mwanachama huyo atakuwa hajatangazwa kufilisika, mkopo huo utapaswa kufuatiliwa na kukusanywa kama mikopo mingine.**

## 12.2 Taratibu za chama kuuza dhamana za mwanachama

Ili kufidia mikopo mibaya chama kinaweza kuuza dhamana za mwanachama. Aidha Kabla chama hakijauza dhamana za mwanachama kitapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

a. Akiba, amana na hisa za hiyari za mwanachama zimechukuliwa katika akaunti ya mwanchama lakini hazijatosheleza kulipa deni husika la mwanchama
b. Wadhamini wamepatiwa taarifa na kushindwa kutoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha deni la mkopaji limelipwa.
c. Ikiwa mwanachama ana dhamana zaidi ya moja dhamana itakayouzwa ni ile tu inayoweza kukidhi deni husika na dhamana zilizobaki zinaweza kurudishwa baada ya kujiridhisha deni husika limelipwa kikamilifu.
d. Chama kitalazimika kurudisha kiasi cha fedha kilichobakia mara baada ya dhamana kuuzwa na kufuta mkopo
e. Chama kinaweza kuuza dhamana za mdhamini baada ya akiba, hisa na dhamana za mkopaji mwenyewe kushindwa kulipia mkopo.

## 13.0 HITIMISHO

Sera hii imeandaliwa na Bodi ya Ngome SACCOS na Kamati ya Usimamizi iliyokasimiwa madaraka kwa niaba ya wanachama kwa barua yenye kumbukumbu Na. MA.82/309/20/14 ya tarehe 05 AGOSTI, 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Mrajis.

Mwenyekiti

Katibu

NGOME SAVING AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LIMITED
NGOME SACCOS LTD
DSR 991
DAR ES SALAAM

TANZANIA
Approved this 01ST
day of MARCH 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies